




Kongamano la Kiswahili
Bayreuth



UNIVERSITÄT
BAYREUTH

Mwaliko wa

KONGAMANO LA KISWAHILI LA THELATHINI NA MBILI

Bayreuth tarehe 31 Mei hadi 2 Juni 2019

Wenzetu wapendwa, wapendwa washiriki, ndugu na marafiki,

Ni furaha yetu kuwaalikeneni nyote kwa Kongamano la Kiswahili la thelathini na mbili!

Tangu hapo mwaka wa 1987, ambapo kongamano la kwanza lilifanyika ili kusherehekea miaka 100 ya ufundishaji wa Kiswahili vyuoni hapa nchini Ujerumani, Kongamano la Kiswahili limepiga hatua nyingi. Kongamano letu ni madhirikano ya kipekee wa kila mwaka yanayofanyika Iwalewa House Chuo Kikuu cha Bayreuth. Mkutano huu unatoa fursa kwa yeyote yule aliye mtaalamu wa masomo mbalimbali yanayohusu utafiti na uchunguzi wa vipengele kadha wa kadha vya lugha ya Kiswahili, fasihi na tamaduni za Afrika Mashariki barani Afrika na Ughaibuni (diaspora). Msingi huu wa kongamano letu mjini Bayreuth, unaojikita katika nyanja na mada maridhawa, huwa ni fursa kwa wengi kujuzana kuhusu tafiti zinazoendelea. Hivyo basi, tunawakaribisheni tena wote ambao huja hapa Bayreuth katika miaka iliyopita na pia tutafurahi sana kuwapokea na kuwakaribisha wataalamu, wanafunzi na mashabiki wapya katika kongamano lijalo.

Mada kuu ya kongamano la 2019

Kongamano hili linalenga kumulika mada kuu ifuatayo: “Pwani na bara”.

Jambo la kutazama/kuunda pwani na bara kama mgawanyiko lina historia ndefu nchini Tanzania, Kenya na Msumbiji. Mgawanyiko huo unaendelea kuunda na kujia siasa za kisasa, maisha ya kila siku na mitazamo kuhusu uhalisia wa jamii. Hakuna linaloakisi mfumo wa kuunda pwani na bara yake bora zaidi kuliko lugha ya Kiswahili: kwa mfano, wakati wa enzi za kikoloni mradi wa kuimarisha lugha isiyofungamana na kikundi moja au kingine pamoja na usambazaji wa fasihi uliofuatana na mradi huo ulichosha ukuzaji wa fasihi isiye ya kikabila; licha na hayo lugha ya kiswahili ilichangia pakubwa kwenye uundaji wa taifa la Tanzania

kuhamasisha michakato ya kuimarisha ukabila iliyoegemea kiitikadi upande wa kukanusha mgawanyiko baina bara na pwani. Kupanua lugha inayotungamana kabila moja tu na kanuni ya kifasihi kwenye mazingira mapana ya taifa linamaanisha kudhoofisha utamaduni wa kimasomo wa pwani: Wakati Kiswahili kimekuwa lugha ya taifa, kiswahili cha pwani kimegeuka kuwa “lahaja” – na zaidi imetengwa na serikali ya kitaifa kama “lugha nyingine za kikabila” au “lugha za mama”.

Tunapenda kualika mawasilisho na michango ambayo yanaakisi kwa makini mitazamo inayopingana baina ya pwani na bara na athari zake katika utendaji wa lugha na utendaji wa kijamii, kwenye sera, uandishi wa kifasihi na kadhalika. Vipi matini na lugha vimetumiwa kufafanua na kuhamasisha maeneo tofauti? Vipi pwani na bara na muungano wa taifa zimesawirika katika maandishi ya kifasihi? Kwa kiasi gani vipengele hivi vinatofautiana baina ya Kenya na Tanzania? Au yanalinganishwaa na michakato ya utofautishaji wa kiitikadi Uganda, Burundi na DRC? Vipi muundo huu umebadilika kwa kupita wakati? Kwa kiwango gani utafiti (wa kimagharibi) umechangia kwenye jambo hilo?

Zaidi za hayo, tunapendekeza mitazamo inayoacha nyuma mgawanyiko huo kulenga si juu ja itikadi bali utendaji wa uandishi, usemaji na maingiliano ya kijamii kutafuta maunganisho na mahusiano baina ya pwani na bara na kupitia maeneo mapana ambamo lugha ya Kiswahili kimetumika. Kwenye miaka ya karibuni, tafiti za Bahari ya Hindi zimeleta mfano wa kuvutia kwa tafiti za kiafrika kwa pendekezo lake la kutotazama Afrika kama bara lililotengwa bali kama bara limeundwa kiuchumi, kiutamaduni na kilugha kwa njia ya mahusiano na mitandao. Tungependa kutumia mtazamo wa mitandao na mahusiano ili tuzingatie mahusiano mbalimbali baina maeneo ya pwani na ya bara, lugha zao na matini za kifasihi – na kuhusisha pia mitazamo juu ja viunganisho vilivyokosekana na jambo lisilolinganishika. Wakati pwani imebahatika kama mahali pedwa pa utafiti, tunakaribisha hasa mawasilisho kutoka bara, sehemu ya ndani ya pwani na “kutoka pembeni” ya eneo Kiswahili linapozungumzwa.

Mada nyingine

Tumependekeza mada hii kuu hapa juu iwe ndiyo mada kuu ya kujengea mijadala yetu kwenye kongamano la 2019, lakini kama mjuavyo, Kongamano la Kiswahili Bayreuth halibani washiriki katika sehemu zilizotajwa tu. Kwa hiyo, pia tunawaulizeni msisite kupendekeza michango mingine ya vipengee vinavyorejelea lugha, fasihi au tamaduni za maeneo ya Kiswahili; kwani Kongamano la Bayreuth linalenga nyanja tofauti tofauti na vile vile ni fursa

iliyo wazi kwa michango yoyote ile inayohusu Kiswahili, Uswahili na Waswahili kwa jumla. **Jopo la kwanza** limeshapendekezwa na Nico Nassenstein na Andrea Hollington: *Sociolinguistic variation and change in Kiswahili: Creative practices, playful language, translocal communication*.

Usajili

Tafadhali tumeni makala katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kila wasilisho litapewa muda wa dakika thelathini tu; ambamo dakika ishirini ni za kuwasilisha na dakika kumi ni za majadiliano na hadhira. Tafadhali jandikishe kwa baruapepe kupitia swahili@uni-bayreuth.de na ututumie kichwa (angaa cha awali) cha makala au mapendekezo ya paneli mpaka **tarehe 30 mwezi wa Oktoba mwaka wa 2018**. Iwapo utawasilisha kwa Kiswahili, tutumie pia muhtasari wa makala kwa Kiingereza. Tunawaomba wote kujiandikisha hata ikiwa mtashiriki bila ya kuwasilisha makala.

Pahala na Wakati

Pahala pa Kongamano hili ni Iwalewahaus, kituo cha masomo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth, iliyoko kwenye Wölfelstraße 2, kuanzia tarehe 31 Mai hadi 2 June 2019.

Wasilianeni nasi bila kusita iwapo mna maswali yoyote. Kwa mambo yote yanayohusu kongamano tafadhali tumieni anwani yake ya barua pepe; yaani swahili@uni-bayreuth.de

Karibuni nyote! Salamu nyingi,

Ni watayarishi wenu

Serena Talento, Nikitta Adjirakor, Annachiara Raia, Duncan Tarrant and Clarissa Vierke

Swahili Colloquium

Prof. Dr. Clarissa Vierke

Literaturen in afrikanischen Sprachen

Universität Bayreuth

95440 Bayreuth

Telefon: + 49 921 55-3550

Fax: + 49 921 55-3641

Email: swahili@uni-bayreuth.de